# Shughuli za kujifunzia nyumbani

UJIFUNZAJI hutokea mahali popote wakati wowote na kwa kila mtu



EENET Enabling Education Network

NAD – The Norwegian Association of Disabled

**EENET – Enabling Education Network**
PO Box 422
Hyde
Cheshire
SK14 9DT
UK

www.eenet.org.uk

info@eenet.org.uk

+44 (0)7929 326 564

This work is licensed under the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License. To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/

Kazi hii iliidhinishwa chini ya the Creative Commons Attribution-Sio ya kuuza-Sambaza ilivyo 4.0 Leseni ya kimataifa. Ili kuona nakala ya leseni hii, tembelea tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by- nc-sa/4.0/

# Yaliyomo


**Utangulizi** 4

**Kurekebisha shughuli kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum ya kielimu na ulemavu** 6

**Orodha ya Shughuli** 8-73

Kitabu cha ABCH 8

Jenga mnara 10

Jenga mchezo wa kuruka vizuizi 11

Mzingile wa namba 13

Kupika chakula huku ukitia maanani idadi ya watu 16

Tengeneza mchezo wa bodi 18

Je, unaona ninachokiona mimi? 20

Chora mnyama wa ajabu 21

Chora mji wako wa kufikiria 23

Vitu unavyopendelea 25

Fanya Boti yako ielee majini 27

Kwenda sokoni 28

Ni maneno mangapi ...? 30

Ningekuwa rais ... 31

Fanya mahojiano na mtu mzima 33

Buni kidude (kifaa au mashine) 35

Ufinyanzi wa sanamu kutokana na takataka 37

Utengenezaji wa orodha 39

Chora ramani ya eneo lako 40

Tengeneza karagosi kutokana na soksi 42

Bao au mchezo sawa wa kuhesabu 44

Kutazama mazingira asilia/ Ulimwengu asilia 46

Wimbo mpya, tuni ya zamani 49

Mashairi ya kipuuzi 50

Panda mbegu na uiangalie inapokua 53

Kusoma pamoja 55

Windo la skavenja 58

Alama ya siri 60

Maumbo na mikondo katika ulimwengu wa asili 62

Duala la hadithi 64

Shukuru shujaa wa Jamii 66

Kuwinda hazina 67

Maswali ishirini 69

Barua kwa mwalimu wako 71

# Utangulizi

## Nyenzo hii ni ya nani?

- Shughuli hizi ziliandaliwa kufaidi **watoto wote**; wenye ulemavu na wasio na ulemavu.
- Shughuli hizi ni za **kila mtu**;- akina mama na akina baba, walezi, wavulana na wasichana, vijana ndugu (akina dada na akina kaka) babu na nyanya, wajomba na shangazi. Kusoma kwa pamoja kuna faida nyingi sana.

## Shughuli hizi ni zipi?

Huu ni **'mchanganyiko wa shughuli** kwa wasichana na wavulana wa miaka yote na wazazi wao, walezi na familia kufanyia nyumbani. Mtu yeyote anaweza kutumia maoni na ubunifu wake kuchangia shughuli hizi. Shughuli zilizo nyingi zinaweza kufanywa mara nyingi na kwa njia tofauti. Shughuli hizi zinatoa msaada kwa njia tofauti ambazo watoto hujifunzia nyumbani. Unaweza kutambua baadhi ya shughuli kwa sababu watoto wako wanazifanya tayari. Shughuli hizi husaidia familia kuelewa zaidi jinsi ujifunzaji unavyotokea nyumbani na jinsi kusomea nyumbani kunavyoweza kusaidia kuboresha ujifunzaji shuleni.

## Kwa nini Shughuli/Mazoezi haya yaliandaliwa?

Shughuli hizi husaidia zile mbinu nyingine nyingi ambazo watoto wanatumia kusomea nyumbani. Unaweza kutambua baadhi ya shughuli hizi kwa sababu tayari watoto wako wanazifanya. Shughuli hizi zinasaidia familia kutambua zaidi jinsi gani **ujifunzaji unavyotokea nyumbani** na jinsi kujifunzia nyumbabi kunavyoweza kusaidia kuboresha kusomea shuleni.

## Jinsi ya kufanya Shughuli/Mazoezi haya?

Pitieni mazoezi haya wewe pamoja na mtoto wako. Mpe nafasi mtoto wako kuchagua mazoezi anayoona kuwa yanavutia. Hakuna mkabala wowote maalum wa kufanya mazoezi haya.

Kuna habari iliyotolewa kuhusu kila zoezi kama ifuatavyo:

> **Zana unazohitaji kuwa nazo:** Kasha hili linaonesha ni maandalizi na zana zipi ambazo zinatakiwa kufanya shughuli hili. Baadhi ya mazoezi hayahitaji vifaa, mengine yanahitaji penseli na karatasi au vifurushi vilivyotumiwa tayari na vitu vingine vinavyoweza kuwa karibu na nyumba na havikugharimu kifedha.

**Mambo ya Kufanya:** Maagizo haya yameandikwa kuwaongoza watoto. Watoto ambao wana uwezo wa kusoma wanaweza kufuata hatua hizi wao wenyewe. Watoto wengine huenda wakahitaji usaidizi wa ziada kutoka kwa ndugu au mtu mzima aliye na uwezo wa kusoma.

**Shughuli za ziada:** Wakati mwingine shughuli za ziada zinaingizwa ndani ya mazoezi kuwapa watoto wakubwa au wale wenye uwezo zaidi changamoto kubwa.

Chini ya kila shughuli/ zoezi, kuna habari ya kukusaidia kuchagua zoezi/shughuli zinazomfaa mtoto wako; hii ni pamoja na:

**Umri**: Hii inapendekeza shughuli gani inafaa kwa kila shughuli. Matokeo yao yanaweza kutofautiana kwa mfano watoto wakubwa wanaweza kuandika mengi au kuchora michoro iliyo wazi wazi au bora zaidi.

**Usaidizi wa Mtu mzima/ndugu:** Hii inaonesha kwamba wewe au kaka au dada yako mkubwa mnaweweza mkamsaidia mtoto kidogo au sana au kama anaweza kufanya kazi peke yake. Habari hii itakusaidia kufanya maamuzi ya kuwa karibu na mtoto wako ukiendelea kufanya shughuli zako huku yeye akifanya zoezi lake. Wakati mwingine, wewe au ndugu yako mnaweza kuwapa msaada wa ziada watoto wenye mahitaji maalumu ya kielimu au ulemavu.

**Mambo ambayo Utajifunza (maarifa) na yale utakayojizoeza (ustadi):** Kila zoezi/shughuli husaidia mtoto kuongezea maarifa yake, kujizoeza au kujifunza ustadi mpya. Kasha lililopo chini ya kila shughuli/zoezi linaonesha maarifa na ustadi unaoshughulikiwa na zoezi hilo. Shughuli zilizo nyingi zinahusu kutengeneza, kujenga au kuunda kitu kinachomsaidia mtoto wako kujizoeza na stadi muhimu. Stadi hizi ni pamoja na mawasiliano, ushirikiano (kufanya kazi na wengine), ubunifu, utatuzi wa matatizo, umakinifu na uratibu wa kimwili. Shule na walimu wanajua ya kwamba stadi hizi ni za umuhimu sana. Watoto wana nafasi nyingi za kusome nyumbani kupitia michezo na kufanya shughuli za kila siku kama vile kupika.

**Njia tofauti za kufanya shughuli/zoezi:** Shughuli zilizo nyingi zinajumuisha maoni ya jinsi ya kurekebisha shughuli kwa mtoto aliye na mahitaji maalum ya kielimu au ulemavu. Shughuli zote zinaweza kufanywa na watoto wote, lakini watoto wengine huenda wakahitaji msaada zaidi au wanaweza kutumia njia tofauti za kufanya shughuli hiyo (kama vile kuchora au kuzungumza badala ya kuandika; au kuirahisisha shughuli). Ukurasa unaofuata unatoa maoni zaidi ya kuzoea shughuli. Unamjua mtoto wako vizuri kwa hivyo unajua ni nini kitakachomfaa.

**Kumbuka kwamba ujifunzaji hutokea mahali popote wakati wowote.**

# Kurekebisha shughuli kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum ya kielimu na ulemavu

Kasha lilopo chini ya kila shughuli/zoezi huonesha namna ya kurekebisha shughuli/zoezi kwa watoto wenye mahitaji maalum ya kielimu na ulemavu. Kila mtoto ni wa kipekee kwa hivyo haya ni maoni ya jumla sana. Mara nyingi mtoto atatuongoza kwa kile anachokipenda yeye. Tunapofanya shughuli/zoezi na watoto tunaboresha uwezo wetu wa kuwasaidia na kujua ni kwenye uwanja gani watoto wetu hufanya vizuri, vitu wanavyopenda kufanya na ni wapi wanahitaji usaidizi.

Ni sawa kumsaidia mtoto wako anapokuwa anafanya shughuli fulani, lakini hakikisha kwamba 'humfanyii' shughuli au mazoezi yake.

-Watoto wanataka kuhisi kana kwamba wamepata mafanikio fulani. Usidhani kuwa mtoto hawezi kufanya zoezi/shughuli. Unaweza kubuni njia za kurekebisha shughuli ili kila mtu aifanye.

Yafuatayo ni mapendekezo zaidi kwa watoto walio na ulemavu kwenye sehemu maalum za miili yao au walio na shida ya kusoma. Mawazo haya yanaweza kutumika katika shughuli zozote zile.

## Watoto wenye matatizo ya kuona

- **Tumia herufi kubwa**: Zoezi/shughuli likijihusisha na kuandika, angalia ikiwa mtoto anaona ni rahisi kusoma herufi kubwa au herufi ndogo. Wakati mwingine herufi ndogo zinafaa zaidi kwa sababu zina 'umbo' iliyo rahisi kusomwa ikilinganishwa na ile ya herufi kubwa; na hivyo ni rahisi kuzisoma na kuzitambua.
- **Tumia Rangi:** Ikiwezekana tumia rangi tofauti tofauti, kuandika maneno ambayo ni ya msingi katika ujenzi wa sentensi (kwa mfano maneno kama 'a' na 'the' na/au vitenzi vya kawaida kama vile 'sema', 'leta' na 'toa'). Hii inaweza kumrahihishia mtoto kusoma au kuandika.
- **Tumia vifaa vya kugusa** kutengenezea na kujengea vitu ili watoto wenye matatizo ya kuona waweze 'kuhisi' na 'kugusa' kitu wanachounda. (Kwa mfano jenga mnara kwa kutumia vitu vilivyotengenezwa kutokana na vifaa mbalimbali.)
- **Elezea picha:** Picha zikiwa sehemu ya shughuli/zoezi, kumbuka kumwelezea mtoto picha hizo.
- Kumbuka, maoni haya yanaweza kuwasaidia watoto wote pia, siyo tu wale walio na shida ya kuona.

## Watoto wenye matatizo ya kusikia

- **Tumia Lugha ya Ishara** ikiwa wewe na mtoto wako mnaifahamu. Au jifuzeni vifungu vya msingi vya lugha ya ishara wewe pamoja na mtoto wako.
- **Mwangalie usoni mtoto ambaye hawezi kusikia vizuri** na useme waziwazi

(Usipige kelele) Tumia **lugha ya mwili, ishara uso na ishara za mikono** kukusaidia kuwasiliana kile unachomanisha.

- Jaribu kufanya shughuli katika maeneo yenye mwanga wa kutosha ili mtoto aweze kupata ujumbe kwa kusoma midomo yako.
- Ongea katika mwendo wa kawaida na usinung'unike.
- Tumia penseli na karatasi (au chaki na ubao) wakati wa shughuli za kuandika au kuchora picha isaidie kueleza jambo. Ikiwezekana, mwoneshe mtoto shughuli badala ya kutegemea maelezo tu (maongezi au lugha ya ishara).
- Kumbuka, baadhi ya maoni haya yanaweza kusaidia watoto wote pia, siyo tu wale wenye matatizo ya kusikia.

## Watoto wenye matatizo ya kutembea

- **Weka nyenzo na vifaa karibu nao:** Hakikisha kwamba vifaa unavyotaka ili kutekeleza shughuli vinawekwa pale mtoto anapoweza kuvifikia kwa urahisi.
- **Jaribu kutumia vifaa vyenye ukubwa unaosaidia watoto kushirikana** (Kwa mfano, penseli kubwa na kalamu zinaweza kuwa rahisi kushikilia)
- **Ongoza na usaidie matendo:** inapohitajika, (kwa mfano, huenda ukahitaji kumsaidia mtoto na mzunguko wa kete wakati wa mchezo wa ubao).
- **Dhibiti Nafasi:** Badilisha shughuli ili ziweze kufanyika katika nafasi ndogo, kwa kutumia mwendo mdogo, (kwa mfano, shughuli za uwindaji wa skavenja au shughuli za uwindaji hazina zinaweza kufanywa katika chumba kimoja badala ya nyumba nzima au nje ya nyumba).

## Watoto ambao wanachukua muda mrefu kujifunza


- **Rahihisha Shughuli** na ushughulikie sehemu yake peke yake (Kwa mfano, imba aya moja tu ya wimbo katika Wimbo Mpya, sauti ya zamani' siyo tatu; andika orodha fupi katika 'Uandikaji wa orodha.' Mtoto wako anaweza pia kuandika neno moja badala ya sentensi nzima kuwasilisha maoni yake)
- **Tumia sana mchoro kuliko Kuandika.** Kazi nyingi tayari zinajihusisha na uchoraji. Kwa zile shughuli zinazomtaka mtoto kuandika, anaweza kuchora maoni badala yake.
- **Yagawe Maagizo** katika hatua rahisi na umwombe mtoto kuyafanya moja baada ya nyingine. (Kwa mfano, 1, chukua penseli na karatasi, 2, Chora umbo 3, Lipake rangi umbo hilo 4, malizia kwa kuliwekea vitambulisho.
- **Rudia Maagizo** mara mbili au mara tatu ili mtoto aweze kuyasikia na kuelewa ujumbe.

Wacha watoto wakuongoze kila wakati. Watakujulisha ikiwa wanaelewa na ikiwa wana nia ya kufanya shughuli hiyo au la. Toa usaidizi kwa upole lakini usiwashinikize watoto.. Mara nyingi inasidia kukiri kuwa shughuli ni ngumu na kisha ukaifanya kuwa shughuli ya pamoja. Unaweza kusema, "Shughuli hiyo ni ngumu kidogo, sivyo? Je, tunaweza tukaifanya pamoja? "

# Kitabu cha ABCH

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli (za rangi ikiwa unazo), karatasi, gundi au sindano na uzi.

## Mambo ya kufanya:




- Andaa karatasi na penseli zenye rangi.
- Utatengeneza kitabu cha alfabeti. Kunja vipande vya karatasi. Je, utahitaji karatasi ngapi?
- Fanya mpango wa jinsi utakavyochora herufi. Herufi moja kwa kila ukurasa? Mbili kwa kila ukurasa?
- Fikiria kuhusu jinsi ya kuchora herufi. Je, zitakuwa herufi kubwa? Herufi zitaonekana kama katuni za watu? Zipake rangi herufi hizo ikiwa unayo.
- Ongeza maneno yanayoanza na herufi ya kialfabeti katika kila ukurasa. Je, utaweka picha za vitu/wanyama ambao majina yao huanza na herufi?
- Chora jalada la kitabu. Kumbuka kuandika jina lako kama 'mtunzi' (mwandishi wa kitabu)
- Kunja kitabu kisha umwombe mtu mzima aushone mgongo wa kitabu kwa uzi na sindano au ukiambatanishe kitabu kwa kutumia gundi.

### Shughuli za ziada:

- Soma au omba mtu fulani akusomee hadithi ifuatayo:

**Mkanganyiko katika nchi ya -Alfabetid**

Siku moja, mapacha 'e' na 'e' waliamua kujifurahisha. Hivyo, waliingia ndani ya maneno waliyoweza kufikiria. Waligeuza neno 'ship' (meli) likawa 'sheep' (kondoo) na kondoo akaloa na kuchanganyikiwa. Waligeuza neno 'chick' (kifaranga) likawa 'cheek' (shavu) na ikamchukulia siku nzima mama kuku kumtafuta mtoto wake. Waligeuza neno 'stir' (koroga) likawa 'steer'(shika usukani) na mpishi hakujua alichokuwa anafanya. Waligeuza neno Will (ridhaa) likawa wheel (gurudumu) akabiringita chini ya mlima. Mapacha walicheka sana. Lakini herufi nyingine hazikuliona hili kama jambo la kuchekesha. Mwishowe mkuu wa herufi zote za kialfabeti alisema, 'sawa imetosha'. Akawaingiza mapacha kati kati mwa neno 'slip'(utelezi) akawasindikiza kwenda kwa sleep (kulala).

- Je, unaweza kutunga hadithi yako mwenyewe kuhusu herufi za Alfabeti?

**Umri**: Shule ya Msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Wastani

**Mambo utakayojifunza**: Alfabeti, ukuzaji wa lugha, msamiati na tahajia

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, kushirikiana, kudizaini

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Tunga wimbo wa alfabeti.
- Omba mtu mwingine akusaidie kutengeneza kitabu.
- Tumia mawe madogo madogo au vizibo vya chupa (ya soda) kutengeneza alfabeti kwenye meza au sakafuni.

# Jenga mnara

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Kadibodi au kifurushi cha plastiki, masanduku madogo, mawe yaliyo sawasawa.

## Mambo ya kufanya:



- Kusanya pamoja vitu vingi vyenye sehemu ya chini iliyo bapa kadri iwezekanavyo. Hivi vinaweza kujumuisha masanduku makuukuu, katoni zenye vizibo, vitabu, mawe madogo yaliyo sawasawa, mitungi ya plastiki yenye vizibo....
- Jaribu kujenga mnara kwa kutumia vitu hivyo. Je, unagundua nini kuhusu vitu gani unaweza kuweka juu ya vingine? Je, vitu vikubwa viko wapi? Je, nini kinatokea unapoweka vitu vidogo chini ya mnara wako?
- Je, unaweza kuujenga mnara wako kwa urefu kiasi gani?
- Nini hupelekea mnara wako kusimama au kuanguka? Unawezaje kuufanya mnara wako kuwa imara?

**Umri:** Shule ya Msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Uwezo wa kusimama au kupanga vitu bila kuanguka, usanifu

**Mambo utakayojizoeza:** Kujaribu, ubunifu, uratibu na ufahamu wa anga

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Ask Omba mtu mwingine akusaidie kujenga mnara wako.
- Ukiwa na matatizo ya kuona, tumia vitu vya kugusa ili uweze kuuhisi mnara.
- Ukiwa na utata kusawazisha vitu vidogo, tumia vitu vikubwa ambavyo vinasawazishwa kwa urahisi.

# Jenga mchezo wa kuruka vizuizi

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Fanicha, vitu vikubwa kama vile kadibodi au vipande vya mbao, matairi makukuu ya gari n.k.

## Mambo ya kufanya:

- Kuruka Vizuizi ni jumla ya vitu ambavyo unafaa kupanda juu ya vitu au kupitia. Inaweza kuhusisha kukimbia, kuruka, kupanda juu ya vitu na kusawazisha.Ukitaka, unaweza kuurahihisha mchezo au kuufanya kuwa mgumu.  Angalia mfano katika picha inayofuata

- Pata nafasi (ndani au nje) unapoweza kutengenezea mchezo wa kuruka vizuizi. Kusanya pamoja vitu vya kutumia katika mchezo wa kuruka vizuizi kwa mfano vipande vya mbao, mawe makubwa ya kutengeneza daraja matairi makukuu, fanicha kukuu. Muulize mtu mzima kwanza ikiwa ni sawa kutumia vitu hivyo.



- Buni na ujenge mchezo wako wa kuruka vizuizi. Mfikirie mtu atakayeucheza mchezo huu. Ufanye kuwa mgumu kiasi mchezo huu kwao lakini usiwe mgumu kupindukia yaani usiowezekana kuchezwa!

- Jaribu mchezo wako wa kuruka vizuizi- kuna kitu chochote ambacho ungependa kubadilisha? Omba mtu fulani ahesabu muda utakaoutumia wakati unapozunguka kizuizi.



**Umri**: Shule ya Msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Kiwango cha Wastani

**Mambo utakayojifunza**: Kubuni, ujenzi

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, utatuzi wa matatizo, ushirikiano wa kimwili, ufahamu wa anga

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**


- Urahihishe mchezo wako wa kuruka vizuizi kwa sababu ya mtu aliye na matatizo ya kutembea au ya kuona. Husisha miendo wanayoweza kufanya kama vile kutambaa au vitu mguso ili waweze kugusa vitu na kuhisi wakiwa wanazunguka.

# Mzingile wa namba


**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli/kalamu na karatasi, chaki

## Mambo ya kufanya:

- Nakili mchoro huu kwenye karatasi au tafuta eneo kubwa ambapo unaweza kuuchora mchoro huo aridhini kwa kutumia chaki.





- This game is about playing with numbers. From the 'START' you move along the lines to the 'FINISH'. You can go in a straight line or zig-zag or any other way along the lines.
- As you move along the lines you make a calculation (sum) using the numbers you pass so you end up with a final number at the FINISH.
- For example: How many different ways can you make the number 8?





**1.**

2 x 4 = 8




**2.**

2 + 2 + 4 = 8




**3.**

3 x 4 – 4 = 8

(12) – 4 = 8

Jibu: kuna njia tatu zinazowezekana

- Kanuni ni:
  - Kila njia lazima iwe tofauti.
  - Hakuna njia inayoweza kupitia kituo zaidi ya mara moja.
  - Kila wakati unapopita namba, lazima utumie alama ya kuongeza, alama ya kutoa na/au alama ya kuzidisha kujumuisha nambari hiyo katika hesabu yako.

- Je, unaweza kupata njia itakayokuongoza hadi kwa nambari 10? Andika hesabu yako. Je, nini kuhusu njia mbili zinazozalisha nambari 16?

- Ni njia gani tofauti na nambari za mwisho unazoweza kuunda? Ni nambari gani kubwa zaidi unayoweza kuunda? Ni nambari gani ndogo zaidi unayoweza kuunda? Unaweza kuunda jumla ya nambari ngapi za mwisho kwa pamoja?

**Shughuli za ziada:**

- Mpe mtu mwingine namba ya mwisho halafu umwombe kutafuta njia. Anawaweza kupata njia ambazo ulikuwa hujazifikiria!

- Badilisha namba zilizo kwenye mchoro na namba zako mwenyewe.

- Namba yoyote inawezekana lakini ni bora zaidi nambari zikibaki za tarakimu moja au mbili

- Unaweza pia kutumia ushuria kuifanya ya kuchochea au ngumu sana.

- Kwa mfano, 0.5 x 4 = 2 au  2.5 x 5 = 12.5.

**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Wastani

**Mambo utakayojifunza**: Mahesabu, kujumlisha, kutoa na kuzidisha

**Mambo utakayojizoeza:** Uwezo wa kutatulia matata, umakinifu, ushirikiano, mawasiliano

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Tenegeneza mzingile mkubwa sakafuni kwa kutumia chaki na 'upitie' kwenye njia ikusaidie kukumbuka vyema hesabu.
- Dhibiti nambari kwenye mchoro, ziwe kati ya 1 na 5.
- Tafuta njia tofauti za kuondoka kutoka kwenye 'Anza' hadi 'Maliza' na uhesabu idadi ya  nambari unazopitia (bila kuzijumulisha kwa pamoja).

# Kupika chakula huku ukitia maanani idadi ya watu

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi, viungo na vyombo vya kupikia.

## Mambo ya kufanya:

- Fanya maamuzi ya kitu ambacho ungependa kupika. Panga mapishi yako na mtu mzima au ndugu yako mkubwa ikiwa unahitaji usaidizi. Andika orodha ya viungo (vitu vya kupikia) ambavyo utahitaji.
- Amua idadi ya watu utakaowapikia. Utahitaji kiasi gani cha kila kiungo kwa idadi hiyo ya watu? Andika bei ya kila kiungo kando ya kiungo kwenye orodha.
- Je, jumla ya pesa ingekuwa kiasi gani ungetakiwa kuwapikia watu wenye wingi wa mara mbili zaidi ya idadi hii? Nusu yao? Watu wawili zaidi?
- Tayarisha viungo na vyombo vya kupikia (viungu au sufuria). Pima viungo.
- Zizungumzie hatua au maagizo ya maelezo ya mapishi na uandike kila hatua. Tumia maneno kama vile, 'katakata', 'menya', 'koroga' na 'changanya' kuelezea upishi.
- Fuata kila hatua ya maelezo ya mapishi kisha ufanye marekebisho ya maagizo yako yaliyoandikwa unapoendelea, jaribu kuwa wazi wazi kadri iwezekanavyo ili mtu mwingine aweze kufuata maelezo yako ya mapishi.
- Unapomaliza kupika, waalike ndugu zako waje kula chakula ambacho umepika.
- Fikiria kuhusu namna utakavyokigawa sawa chakula chako kwa idadi ya watu walioko. Je, kila mtu atapata vijiko/ vipande vingapi? Je, kuna chakula cha kutosha kwa watu kula mara mbili?

## Shughuli za ziada:

- Andika maelezo ya mapishi malidadi kabisa ili mtu mwingine aweze kufuata maelekezo hayo. Mwombe atengeneze mapishi kisha akwambie jinsi maagizo yalivyokuwa wazi na ikiwa kuna mabadiliko yoyote yanayopaswa kufanywa.




- Chagua maelekezo ya mapishi ambapo unaweza kugawanya matokeo ili utenge visehemu, kama keki au biskuti au kukata matunda kwa saladi ya matunda. Tengeneza sehemu ndogo na uziandike (kama picha hapo juu).

- Andika kitabu cha maelezo ya mapishi ya vyakula vyote unavyopenda kupika.

**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Wastani / unahitajiwa sana

**Mambo utakayojifunza**: Hesabu, hisbati ya matumizi, kupima, kupanga mapishi, ukukuzaji wa lugha.

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, mawasiliano, utatuzi wa matatizo, umakinifu, ushirikiano

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**


- Mwombe mtu mwingine akusaidie katika zoezi zima la kupika.
- Chagua kazi za kupika unazoweza kufanya. Je, unaweza kukoroga? Unaweza kutia viungo kwenye chakula?
- Toa maagizo kwa njia ya maneno badala ya maandishi.
- Mwombe mtu mwingine aandike maagizo.
- Chora michoro ya kila hatua ya mapishi.

# Tengeneza mchezo wa bodi

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu zenye rangi, karatasi kubwa, vitu vidogo, mkasi, dadu au dadu ya karatasi iliyotengenezewa nyumbani.

## Mambo ya kufanya:

- Tayarisha karatasi na penseli, za rangi tofauti tofauti ikiwezekana. Weka kipande kikubwa cha karatasi iliyo wazi kwenye meza au sakafuni.




- Chora njia ya miguu inayopindapinda kwenye karatasi. Igawe katika miraba.

- Chagua upande mmoja wa mwisho kuwa mwanzo na upande mwingine kuwa kimalizio. (Angalia mchoro wa chini).

- Andika neno'pata kadi' kwenye baadhi ya miraba. Kwenye baadhi ya miraba andika, 'rudi kwenye nafasi' au 'kosa zamu'.Je, una mawazo mengine juu ya jinsi kuwaongoza tena wachezaji mbele na nyuma? Acha wazi miraba iliyo mingi kwenye bodi. Unahitaji zoezi gumu zaidi kufanya mambo yaendelee kuwa ya kupendeza lakini usiwe mgumu sana ukawa mgumu wa kushindwa.

- Ili kutengeneza kadi, kata miraba midogo ya karatasi. Andika agizo/ shughuli kwenye upande mmoja wa kila mraba mdogo. Kuwa mbunifu ujaribu kuwa na mchanganyiko wa aina tofauti za maagizo! Kwa mfano:

- Ukweli wa hisbati: hesabu katika 3, 6, 8 ...
- Matendo ya kimwili: zunguka mara tatu, piga kikofi vichwa vyetu na kufikicha tumbo lako ukihesabu hadi ishirini.
- Andika orodha ya maneno yenye vina.
- Imba Wimbo.
- Maarifa ya jumla: Taja miji mikuu 5 ...

- Nani atacheza na wewe? Mtu mmoja? Zaidi? Mpatie kila mtu kitu kidogo cha kutembea nacho katika njia ya miguu.
- Kubaliana na wachezaji wengine kuhusu baadhi ya kanuni za kucheza, nani atatangulia kucheza? Kutatokea nini mtu akishindwa kufanya shughuli fulani? Je, unaweza kuomba usaidizi? Unaweza kuruka zamu? Baada ya kukubaliana juu ya kanuni, sasa ni muda wa kucheza.
- Ziweke kadi za 'shughuli' ziangalie chini kando ya mchezo wa bodi. Kila mchezaji anachukua zamu ya kuzungusha kete. Mchezaji anahamisha kitu chake kwenye njia idadi sawa ya mraba kama idadi kwenye kete.
- Wanatua wapi? Fanya kile kinachosemwa kwenye mraba. Wakati mchezaji anatua kwenye 'pata kadi', chukua kadi ya shughuli. Fanya kazi kwenye kadi. Ikiwa mchezaji hawezi, rejea sheria zako za kucheza. Mchezaji anayetangulia kufika mwisho/hitimisho ndiye mshindi.

**Umri**: Miaka minane kwenda juu

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Wastani

**Mambo utakayojifunza**: Ukuzaji lugha, Matumizi ya tarakimu

**Mambo utakayojizoeza:** Mawasiliano, ushirikiano, umakinifu, ubunifu

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Ungana na mtu mzima ili mcheze pamoja.
- Urahihishe mchezo kwa kuondoa baadhi ya miraba.
- Chora njia ya miguu sakafuni kwa kutumia chaki ili uweze kutembea kwenye 'ubao wa michezo'.

# Je, unaona ninachokiona mimi?

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi

**Mambo ya kufanya:**

- Chora picha.
- Inayofuata, andika maagizo ya jinsi ya kuchora picha
- Omba mtu mwingine kufuata maagizo yako bila kumruhusu kuona mchoro wako.
- Akimaliza, linganisha michoro yako na yake. Unaonaje? Michoro hiyo inafanana au ni tofauti? Kwa nini ni tofauti? Je, ni kitu gani ambacho kimeipelekea michoro hiyo kuonekana sawa?

**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza**: Kukuza lugha, kuandika maagizo

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, ushirikiano, mawasiliano


**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Sema maagizo yako badala ya kuyaandika
- Igiza picha yako.
- Tengeneza 'picha' na udongo wa mfinyanzi au ichore kwenye mchanga/ matope

# Chora mnyama wa ajabu

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli zenye za rangi au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:




- Tayarisha  karatasi na penseli, ikiwezekana,rangi chache tofauti.
- Fikiria kwamba paka alikuwa na mkonga kama tembo? Au mbwa alikuwa na ganda? Hilo lingeonekanaje?
- Chora mnyama wako binafsi wa kuwaza mwenye sehemu tofauti za wanyama. Weka kitambulisho chenye maelezo ya sehemu za mnyama.
- Mpe jina mnyama wako wa ajabu.  Jina linaweza kuwa kidokezo kwa wanyama tofauti ambao umetumia kukuongoza katika mchoro wako.

## Shughuli za ziada:

- **Fikiria:** Mnyama huyo anaishi wapi? Je, anaishi katika dunia halisi au dunia nyingine? Je, dunia ya aina gani?  Je, anakula chakula gani?  Je, anatoa mlio wa aina gani? Anatembea vipi? Mnyama huyo alipataje sehemu zake tofauti tofauti za wanyama?
- **Simulia/andika hadithi** kuhusu mnyama
- **Soma hadithi Ifuatayo** (au mwombe mtu mwingine akusomee) ili akupe maoni.

## Fisi na Sungura

Fisi alikuwa akiuza mboga sokoni na Sungura alikuwa akimchokoza sana. 'Huwezi kukimbia haraka kama nifanyavyo mimi, unaeweza? Sungura alimchokoza Fisi. 'Wewe ni mzee na huwezi hata kuona vizuri.'

Sungura alimzunguka Fisi huku akicheza. Fisi alijaribu kumshika Sungura lakini hakuweza. Alikimbia akicheka.

'Siku moja nitamwonyesha' aliwaza Fisi. Hivyo, alijifanya kipofu na kuvaa miwani ya rangi nyeusi.

Sungura alikuwa mfidhuli sana na mjasiri zaidi akendelea kasogea karibu sana na Fisi. Ndipo, siku moja, Fisi akatoa wayo na makucha yake na akamshika Sungura kwa masikio. Hakumruhusu kuondoka. Fisi alijifanya kumla masikio Sungura. Sungura alijipindapinda akatetemeka lakini Fisi akaendelea kumpeperusha juu na chini akiwa ameshikilia masikio yake. Masikio ya Sungura yalirefuka yakarefuka mpaka mwishowe, kwa mvuto mkali, Sungura alijiondoa kutoka kwenye taya za Fisi (meno ya Mzee Fisi hayakuwa mazuri). Sungura alikimbia kwa kasi iwezekanavyo akaenda huko mbali na soko, mbali na mji,mbali na Fisi. Na hiyo ndiyo sababu iliyowapelekea Sungura kuwa masikio marefu.

**Umri**: Shule ya Msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Maumbo na rangi, lugha ya kimaelezo

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, mshikamano

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Toa maelezo ya sura ya mnyama. Omba mtu mwingine kumchora mnyama huyo.
- Tumia udongo wa mfinyanzi au machupa yaliyokwisha tumiwa na vifurushi vya vyakula kutengeneza mnyama.

# Chora mji wako wa kufikiria

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Karatasi na penseli/penseli zenye rangi

**Mambo ya kufanya:**

- Tayarisha karatasi kubwa na penseli.
- Omba mtu akusomee yafuatayo pole pole kwa sauti ili uweze kufunga macho yako na kufikiria.

  Fumba macho yako ufikirie mji wako. Fikiria kwamba unatembea katika barabara ya mji wako wa kubuni. Mji wako unafananaje? Je, mji huo una majengo gani? Majengo yana urefu gani? Kuna aina gani ya usafiri? Je, kuna kituo cha reli? Je, ni mji wenye majini na mti pamoja na maeneo ya kupumzika? Au ni mji wa kisasa wenye barabara zinazopita juu na magari yanayoruka? Chukua dakika chache kuufikiria mji wako.

- Fungua macho yako. Chora mji wako. Panga mahali ambapo majengo yatajengwa na vitu gani vya kuingiza ndani. Orodhesha kwanza kisha umalizie mengine.Tumia rangi ukiwa unazo.
- Mji wako utaupa jina gani?
- Angalia mji wako tena. Je, umesahau kitu chochote? Mahali pa maombi? Ng'ome ya zamani au jumba la makumbusho? Mto na mahali pa kuchezea je? Je, watu wanaweza kulizunguka jiji kwa urahisi? Vipi kuhusu watu wenye ulemavu? Upanue mji wako ili uongezee vitu hivi.




**Umri**: Shule ya Msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Wastani

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha, skeli, namna miji mikuu inavyoshughulikia kazi zao.

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, uwekaji mipango, kupanga, kubuni, utatuzi wa matatizo.

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Mtolee maagizo mtu mwingine ya kitu unachotaka yeye akuchoree.
- Jenga mji wako na masanduku matupu, katoni, vijiti na mawe.
- Chora mashamba au miji midogo badala ya mji mkuu

# Vitu unavyopendelea

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi na rangi tofauti tofauti

## Mambo ya kufanya:

- Weka kiganja chako katikati ya karatasi halafu ukichore kwa kukizungushia kalamu.
- Kwenye umbo la kidole gumba chako, andika rangi unayoipenda. Je, kidole gumba hicho utakipaka rangi pia?
- Katika vidole vyako vingine, andika somo unalolipenda, chakula unachopenda, mchezo unaopenda na mnyama unayempenda.
- Upambe mwanya uliobaki na picha za vitu unavyopenda!



### Shughuli za ziada:

- Tafuta vitu tofauti vya kuandika kwenye vidole vyako, vinaweza kuwa vitu vingine unavyopenda sana au kategoria ya maneno kama vile miji mikuu, fanicha zilizomo katika nyumba yako, mambo unayopenda kufanya na kadhalika.



**Umri**: Shule ya msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, ushirikiano

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Mwombe mtu mwingine kwa kutumia penseli achore kuzungushia kiganja chako.
- Mwambie mtu mwingine vitu ambavyo unapenda, umwombe akuandikie vitu hivyo.
- Fikiria vitu vingine vya kuongezea kwenye orodha ya vitu unavyopenda.

# Fanya Boti yako ielee majini

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Mapipa ya plastiki yaliyotumiwa, karatasi au kitambaa, mawe

## Mambo ya kufanya:

- Tafuta beseni kuukuu ya plastiki au machupa ya plastiki kuwa boti yako. Tengeneza boti yako, je utaweka tanga?
- Elea boti yako katika ndoo ya maji au bwawa dogo. Je, boti hiyo inaeleaje kwenye maji? Unaweza kuifanya kuelea kupita maji?
- Kusanya mawe. Je, boti yako itabeba mawe mangapi hadi itakapozama ndani ya maji?



## Shughuli za ziada:

- Unaweza kutengeneza boti kutokana na nyenzo tofauti tofauti? Karatasi kwa mfano? Je,hii inabadilisha kiasi cha mawe boti itakachobeba?

**Umri**: Shule ya Msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo / wastani

**Mambo utakayojifunza:** Sayansi (Fizikia), uzito wa vitu

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, uratibu, mtindo

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Fanya majaribio ya vyombo na vitu tofauti kuona ikiwa vinaelea au kuzama.
- Fanya zoezi hili ukiwa kwenye sinki bafuni au jikoni.

# Kwenda sokoni

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Bidhaa za 'kuuza' katika genge lako, penseli na karatasi, mawe au vifuniko vya chupa

## Mambo ya kufanya:

- Tafuta nafasi pa kuweka genge lako la kisingizio. Inaweza ikawa meza ndogo au nafasi ndogo sakafuni pahali popote.
- Fanya maamuzi kuhusu aina ya bidhaa utakazouza katika genge lako. Chakula? Nguo? Vitabu? Au mchanganyiko wa bidhaa?
- Kusanya bidhaa za kuuza katika genge lako. Omba mtu mzima au ndugu yako mkubwa ikiwa ni sawa kuazima vitu kwanza. Unaweza pia kutumia mawe, vifungo, vifuniko vya chupa, majani, vitawi kama bidhaa za kuuza.
- Tumia mawe au vifuniko vya chupa kama pesa za kujisingizia. Tafuta kisanduku kidogo cha kuhifadhia pesa. Andaa karatasi na penseli ili ujue nini utabadilisha.
- Fungua duka lako. Andika bei ya kila bidhaa kwenye vipande vya karatasi kisha uviweke kando ya bidhaa kwenye genge lako.
- Nani atakuja katika duka lako? Ndugu zako? Watu katika familia yako? Fungua duka lako uwaite wateja waje waingie.
- Ifanye iwe ya kupendeza kwa kukosa bidhaa wanazotaka kununua kila mara. Wape vitu vingine badala yake. Au pandisha bei ya vitu uwaelezee wateja wako kwa nini umepandisha bei? Je, wanakubali upandishaji wa bei huo?



**Umri**: Shule ya Msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Wastani

**Mambo utakayojifunza:** Kuongeza na kutoa na kuhesabu gharama ya punguzo ya bei, lugha ya ununuzi na ya uuzaji.

**Mambo utakayojizoeza:** Mawasiliano, kupatana bei , ushirikiano, ubunifu, utatuzi wa matatizo.

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Shirikiana na ndugu au mtu mzima kutengeneza vitambulisho vya bei.
- Chukua zamu na mtu kufanya kama muuzaduka na mteja

# Ni maneno mangapi ...?

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Andika sentensi kwa Kingereza 'Learning at home is fun'.
- Angalia ni maneno mangapi tofauti katika Kiingereza unayoweza kutunga kutokana na sentensi na kuyaandikia orodha kwa mfano: Learn, ring, night.
- Unaweza kutunga sentensi mpya kwa Kiingereza kutokana na orodha yako ya maneno?
- Fikiria sentensi moja katika lugha yako ya mama uone ni maneno mangapi unayoweza kutunga. Inaweza kuwa sentensi hiyo hiyo au sentensi nyingine.
- Angalia sentensi ya Kingereza ifuatayo ambayo inatumia kila herufi ya alfabeti: 'The quick brown fox jumps over the lazy dog.'
- Unaweza kutunga sentensi katika lugha yako ya mama ambayo inatumia herufi zote za alfabeti?

## Shughuli za ziada:

- Tenegeneza mchezo wa maneno kwa kutumia maneno. Tunga na uandike hadithi fupi kwa kutumia maneno mapya.

**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Kuandika, tahajia, muundo wa sentensi

**Mambo utakayojizoeza:** Kuratibu, uratibu, ubunifu

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Chora picha za maneno badala ya kuandika.
- Mwambie mtu mwingine maneno ili aweze kukusaidia kuyaandika.

# Ningekuwa rais ...

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Fikiria kuwa wewe ni rais wa nchi yako. Ni kitu gani ambacho ungebadilishi kwanza? Je, ungependa kufanya nini kuhusu yafuatayo:
  - Elimu (kwa mfano, shule na walimu)
  - Mazingira (kwa mfano, kulinda uasili)
  - Afya (kwa mfano, hospitali, madaktari na nesi)
  - Usafiri (kwa mfano, jinsi watu wanavyosafiri kwenda hapa na pale)
- Kuna makundi yoyote ya watu ambayo ungependa kusaidia? Je, ni kina nani hao? Utawasaidiaje?



- Nakili sentensi hizi kisha uzikamilishe kwa maneno yako mwenyewe.

## Ningekuwa rais … kwa (jina lako)

Ningekuwa rais wa (nchi yako), Ninge ……………………………
kisha ninge ……………………………

Kungekuwa ……………………………

Ningekomesha ……………………………

THakungekuwepo tena ……………………………

Ningehakikisha kwam ……………………………

Sahihi: ____________________

- Ongezea sentensi nyingi za ziada upendavyo.
- Igiza hotuba ya rais kwa kuzisoma sentensi zako kwa sauti na kwa kujiamini.

**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ujifunzaji wa lugha, Sarufi

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, Umakinifu, Mawasiliano, Kuzungumza kwa Umma

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Omba mtu akusaidie kuandika sentensi zako.
- Chora michoro ya vitu ambavyo unataka kubadilisha.
- Fikiria kuwa wewe ni chifu wa kijiji, meya au mwanasiasa wa kawaida.
- Alika familia yako kukuuliza maswali kisha ujibu katika jukumu la rais.

# Fanya mahojiano na mtu mzima

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi

**Mambo ya kufanya:**

- Fikiria mzee mwenye kupendeza ambaye ungependa kuhoji. Anaweza kuwa mtu katika familia yako au katika jamii yako.
- Ni mambo gani yanayompelekea kuwa mtu wa kuvutia? Je, unataka kumuuliza kuhusu nini? Unataka kumuuliza kuhusu utoto wake? Mabadiliko ambayo ameona? Kuhusu mambo mahsusi alioyapitia?
- Andika maswali unayotaka kuuliza. Chunguza maswali kisha uyapange katika mpangilio ambao ungetaka kuyauliza.
- Fanya mahojiano ya mazoezi na mtu mwingine mzima au ndugu yako mkubwa. Hii itakusaidia kuona ikiwa unataka kubadilisha chochote. Je, mhojiwa alifikiri ya kwamba ulikuwa mzuri? Ulikuwa mtu asiyetani? Mhojiwa alihitaji muda kukwambia mengi zaidi?
- Fanya marekebisho yoyote yale ambayo unafikiri unahitaji kufanya baada ya mazoezi yako. Unahitaji maswali zaidi? Machache? Unataka kubadilisha maswali yoyote?
- Fanya mahojiano. Mshukuru mhojiwa kwa muda wake.

**Shughuli za ziada:**

- Andika mahojiano kama maandishi yatakayotangazwa katika rediyo na/au makala kwa gazeti.




**Umri**: Miaka minane kwendelea

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ujifunzaji wa Lugha, Kujifunza juu ya historia ya familia au jamii.

**Mambo utakayojizoeza:** Mawasiliano, kuandaa na kupanga mahojiano, umakinifu.

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Mwombe mtu fulani akuhoji kwanza ili ujue mambo ya kuuliza.
- Andika maswali ya mahojiano katika herufi kubwa ili yaweze kutambulika kwa urahisi.
- Fupisha maswali ili yawe rahisi kukumbuka.
- Mwombe mhojiwa atoe majibu yake katika sentensi fupi ili yaweze kuandikwa kwa urahisi

# Buni kidude (kifaa au mashine)

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Fikiria kidude (kifaa au mashine) unachopenda kubuni. Je, kidude hicho kinafanya kazi gani? Labda ni kifaa kinachowahudumia watu? Unaweza kusafiri nacho? Je, kimetengenezwa kutokana nyenzo gani? Je, kidude hicho kinatumia umeme?

- Chora kidude chako ulichokibuni na uoneshe sehemu zake tofauti. Je, sehemu zake tofauti zinafanya kazi gani?

- Andika habari kuhusu kidude chako. Je, unaweza kuelezea namna kidude hicho kinavyofanya kazi? Je, unaweza kukitumia kidude hicho kufanya kazi gani?

## Shughuli za ziada:

- Tengeneza kidude chako kutokana na nyenzo zilizotengenezwa upya. Kwa mfano, tafuta masanduku makuukuu na machupa ya plastiki. Andika kwenye sehemu mbalimbali za kidude chako ukipenda kufanya hivyo.

- Tunga tangazo la kidude chako. Ni vitu gani vinavyowavuta wanunuzi kununua kidude chako? Kidude chako kinafanya kazi gani itakayowapelekea watu kukinunua? Kidude chako kitaboreshaje maisha ya watu? Je, kinauzwa kwa bei gani? Andika tangazo la kuwekwa gazetini.



**Umri**: Shule ya Msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha, kuandika na tahajia.

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, utatuzi wa matatizo, umakinifu, mawasiliano, ujuzi wa anga.

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Omba mtu mwingine akuchoree picha.
- Tengeneza kidude chako kutokana na udongo wa mfinyanzi.
- Omba mtu fulani akusaidie kuandika kitambulisho.

# Ufinyanzi wa sanamu kutokana na takataka

**Zana utakazohitaji kuwa nazo**: Vitu vilivyotengenezwa upya na vifurushi, penseli au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Kusanya vitu vilivyotengenezwa upya na vifurushi. Hivi vinaweza kujumuisha machupa ya plastiki yaliyokwishatumiwa, vizibo vya chupa, masanduku ya kadibodi yenye saizi zote, katoni, nguo kuukuu na kadhalika.

- Pia, tafuta bidhaa asiri ambazo unaweza kutumia kukusaidia katika ufinyanzi wa sanamu kutokana na takataka, kwa mfano, vijiti, mawe, majani makavu au udongo wa mfinyanzi au matope.







- Fikiria kitu ambacho ungependa kutengeneza. Mwanaserere? Je, kina magurudumu? Au tundu? Ina kuta? Fikiria umbo la kitu unachotaka kubuni.

- Chora mchoro wa kielelezo chako na upange kitu unachopenda kutengeneza kutokana na kielelezo hicho.

- Tengeneza sanamu yako.

- Angalia sanamu yako tena. Je, unawezaje kuiboresha sanamu hiyo? Ni kitu gani ambacho kingeimarisha sanamu hiyo? Kukisaidia kuwa bora?

**Umri**: Shule ya Msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Kielelezo, umakanika, ujenzi

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, utatuzi wa matatizo, ushirikiano, ufahamu wa anga

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Omba mtu akusaidie kutengeneza sanamu yako.
- Hakikisha ya kwamba dizaini inabaki nyepesi- tengeneza chumgu cha kuwekea mmea, kitu kinachoweza kubingirika au mchezo wa kuhesabu.

# Utengenezaji wa orodha

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Fikiria juu ya vitu kadhaa ambavyo unaweza kuviingiza katika orodha yako:
  - Nyimbo unazopenda.
  - Mimea iliyoko kwenye eneo lako.
  - Vitu vinavyokufurahisha wewe.
  - Vitu ulivyo na uhodari mkubwa.
  - Vitu unavyohitaji  kwa matumizi ya familia yako.
- Jaribu kufikiria orodha nyingine zisizohusu  'vitu ambavyo unamshukuru Mungu kuwa navyo au 'vitu ambavyo unafurahia kufanya'
- Chagua moja ya kategoria na uorodheshe.
- Je, unaweza kuigawanya orodha hii katika orodha ndogo? Kwa mfano, mimea katika eneo lako inaweza kugawanywa katika ile inayoweza kuliwa na ile ambayo hailiwi.

**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha, kuandika, tahajia.

**Mambo utakayojizoeza:** Kupanga, mpangilio, ubunifu, utaratibu.

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**


- Omba mtu akusaidie kuandika orodha.
- Andika orodha yako.
- Kusanya pamoja vitu 10 vinavyofanana. Je, vyote vinatoka shambani? Vyote ni vitu vya kuvaliwa? Vyote vinatoka jikoni? Omba mtu akuandikie majina ya vitu hivi.

# Chora ramani ya eneo lako

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi, viungo vya mapishi na vyombo vya kupikia

## Mambo ya kufanya:

- Tayarisha karatasi na penseli pamoja na kalamu za rangi tofauti tofauti.
- Tembea kuzunguka mtaa wako. Je, unaona nini? (Nyumba, majengo na barabara lakini pia miti au sehemu maalum kama vile makanisa, misikiti au nafasi za kuchezea.)
- Fikiria juu ya urefu wa baadhi ya barabara, je zina urefu gani, baadhi ya miti au majengo yana urefu gani? Na nafasi zilizo wazi kama vile nyanja au misitu je? Masoko?, Shule? Mambo mengine yoyote unayoweza kufikiria?




- Fanya maamuzi ya jinsi utakavyochora ramani yako. Je, utavipaka rangi vitu tofauti? Utaichora yote? Utaweka ufumbuzi kuwakilisha vitu vingine (kama mstari mawimbi wa mto, duala la kijani la mti)?

- Karatasi yako itatakana kuwa kubwa kiasi gani? Karatasi moja tu? Au karatasi mbili?

- Kila kitu kinafaa kuwa na ukubwa au udogo gani? Shule, uwanja wa michezo, barabara au barabara ndogo, masoko yana ukubwa gani?

- Chora ramani. Onesha sehemu/maeneo mbalimbali au uweke ufumbuzi/sherehe.

**Shughuli za ziada:**

- **Fikiria:** Mgeni katika mtaa wako anakuuliza njia ya kwenda sokoni au mtoni. Andika au mweleKeze njia. Tafuta mtu wa kuangalia ramani yako na kuuliza njia.

- **Simulia/Andika hadithi** kuhusu mahali mahususi mtaani. Shule ilianza lini? Je, kulikuwepo na mahali pa kuchezea? Kulitokea janga kama vile mafuriko ya maji au pepo mkali uliotokea katika eneo lako? Na sherehe je? Kuna historia yoyote muhimu? Kuna hadithi ya mizuka ya kusimulia kuhusu eneo fulani?

- **Tengeneza Sanamu** ya mtaa. Tumia vifurushi vikuukuu au masanduku madogo unayoweza kupata pande zote. Unaweza kuiunda sanamu hiyo ili mtu asiyeona aweze kuihisi na kupata njia? Utumiaji wa Kamba unaweza kusaidia.

**Umri**: Miaka

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Wastani/mkubwa

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha, msamiati wa mahali, lugha ya maelekezo, mitaa, alama muhimu.

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, uratibu, kuchora kwa kuzingatia vipimo, uwakilishi, ufahamu wa anga, kuangalia.

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Elezea eneo na umwombe mtu fulani akusaidie kuchora ramani.
- Tengeneza sanamu (badala ya ramani) ya eneo.
- Tengeneza ramani ya nyumba yako au ya chumba kimoja kwenye nyumba.
- Simulia hadithi kuhusu mahali unapoishi na uombe mtu aviandike.

# Tengeneza karagosi kutokana na soksi

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Soksi kukuu, safi na ndefu, kalamu au chaki kubwa, vifungo vikukuu, sindano, uzi na mkasi, sufu

## Mambo ya kufanya:

- Tafuta soksi kuukuu ndefu. Ingiza mkono wako ndani yake utengeneze umbo CH kwa kutumia vidole na kidole gumba chako. Ingiza kidole gumba chako kwenye kisigino cha soksi. Ichezeshe hadi itakavyoonekana kama kichwa chenye mdomo.

- Tumia kalamu au chaki kuweka alama ya pahali macho yatakapokuwa. .  Ondoa soksi. Chora macho mawili au ushone vifungo katika eneo ulipoweka alama ya macho.

- Ongeza sufu kutengeneza nywele. Ili kufanya hili, kata vipande vidogo vya sufu vilivyo na  urefu sawa uvifunge katikati. Halafu vishone kwenye soksi, juu ya macho.

- Pamba karagosi yako ya soksi. Ivishe kofia ndogo au tengeneza mdomo wake kutokana na kadi au kitambaa.

- Ipe jina, karagosi yako ya soksi na ufanye mazoezi ya kuiongelesha. Ifanye kuonekana ya kuchekesha au yenye huzuni kwa namna unavyosogeza mkono wako.  Ifanye ionekane imeshangaa kwa kutenga macho yake au imekasirika kwa kuleta macho yake karibu au kuyafanya macho yakaribiane.

## Shughuli za ziada:

- Tengeneza karagosi nyingine ya soksi na uzifanye ‘zizungumze’ Je, zina tabia gani?  Zinafanya vituko gani? Wape familia yako shoo ya karagoosi.



**Umri**: Shule ya Msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Wastani

**Mambo utakayojifunza:** Uchoraji, mazungumzo, ukuzaji wa lugha

**Mambo utakayojizoeza:** Uratibu, ubunifu, ufaraguzi

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Omba mtu mwingine akusaidie kupamba karagosi yako.

# Bao au mchezo sawa wa kuhesabu

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Mawe, maharagwe au mbegu.

## Mambo ya kufanya:

- Mna michezo gani ya kuhesabu katika nchi yako? Mna michezo yoyote inayochezwa kwa kutumia mawe madogo, maharagwe yaliyokauka, mbegu au sarafu nyingine na bodi (sawa na huu unaooneshwa chini)?
- Mnauchezaje mchezo huo? Je, unajua sheria za mchezo? Ikiwa hujui, unaweza kutafuta mtu ambaye anaweza kukufundisha mchezo huo?
- Ikiwa huna bodi tayari, unaweza kutengeneza moja ardhini? Unaweza kushima mashimo madogo au machimbo ardhini na ukusanye mawe madogo ya kutumia.
- Cheza mchezo. Ikiwa unahitaji wachezaji wawili, utahitaji kupata mtu wa kucheza naye. Kitu gani kinaupelekea mchezo huu kuwa mchezo mzuri?





**Shughuli za ziada:**

- Unaweza kuandika maagizo ya mchezo wako? Fikiria kuwa maagizo ni ya mtu ambaye hajawahi kuucheza mchezo huo.
- Unaweza kuanza mchezo mpya wa kuhesabu? Mfundishe mtu mwingine mchezo wako. . Je, ni mchezo huu unaongozwa na sheria gani?

**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Hesabu, ukuzaji wa lugha (maagizo)

**Mambo utakayojizoeza:** Ushirikiano, utatuzi wa matatizo, mawasiliano, mikakati

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Ikiwa ni vigumu kuokota vitu vidogo, tumia mawe makubwa.

# Kutazama mazingira asilia/ Ulimwengu asilia

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:

- Toka nje na uamue kitu gani ungependa kutazama. Inaweza kuwa mdudu kama buibui akijenga utando wake au chungu akibeba chakula kinywani mwake. Inaweza kuwa mdudu kama kipepeo, ndege au nyuki anayekusanya poleni. Au unaweza kutazama miti na vivuli inavyovirusha upeponi au mwanga juu ya maji kwenye kijito.

- Tazama kwa angalau dakika kumi na tano au zaidi uandike kila kitu unachoweza kuandika. Angalia namna inavyotembea, kuna nyayo za kipekee au rangi (Angalia miondoko yake, kuna alama yoyote mahsusu au rangi za onyo zinazong'aa au rangi zinazoiruhusu kuchanganywa na sehemu ya nyuma). Unaweza kukielezea?

- Jiulize maswali mengine. Ni mkubwa kiasi gani? Je, ana miguu mingapi? Anatembeaje? (Haraka, pole pole, mwendo usio na stadi, vizuri), Je, anaelekea wapi? Kuna nini njiani mwake, anajaribu kufanya nini? Kuna wadudu/ wanyama wengine hapokaribu wanaomfanana? Je, wanyama/wadudu hao wanafanya nini?





**Shughuli za ziada:**

- **Chora** mchoro wa kitu ulichoona.
- **Gundua habari** zaidi kuhusu yale uliyoona. Uliza mtu anayejua kuhusu mambo haya na fikiria swali la kuuliza. Je, mnyama/mdudu anakula nini? Je, kuna aina ngapi za wanyama/mdudu humo? Wanapataje chakula? Wanaishi katika makundi au kila mmoja anaishi peke yake. Je, wanazaa vipi watoto wao? Je, wanahama?
- **Tengeneza Shajala ya uasili.** Hii inaweza kuwa karatasi unakoandika au kuchora yale unayoyaona kila siku. Ukiangalia kitu kile kile kwa siku nyingi (kama vile vivuli miti inavyounza au ua ambalo limefungua au mto, kisha chunguza nini kimebadilika katika siku tofauti.



**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha, lugha ya maelezo, sayansi: ulimwengu wa asili na biolojia.

**Mambo utakayojizoeza:** Kuchunguza kwa uangalifu na kwa karibu. Kujifunza juu ya kile unachoona. Uvumilivu, umakinifu, mawasiliano.

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Ukiwa na matatizo ya kuona, tumia hisi zako nyingine kuhisi asili. Sikiliza, nusa na uguse ardhi, miti na mimea inayokuzunguka.
- Elezea unachonusa, sikia au hisi. Sema/Soma kwa sauti maelezo yako kwa mtu mwingine kuandika.
- Chora michoro badala ya kuandika notisi au omba mtu mwingine kukuandikia mawazo yako.

# Wimbo mpya, tuni ya zamani

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** hamna

## Mambo ya kufanya:

- Fikiria wimbo katika lugha yako ya mama ambao kila mtu anajua na ni rahisi kuimba
- Tumia maneno mapya katika tuni ile ile. Unaweza kutunga wimbo kuhusu jambo lolote unalotaka, mfano, jinsi ya kupiga mswaki meno yako, mhusika wa hadithi unayempenda, au jambo la kuchekesha lililotokea.
- Fundisha watu wengine wimbo huo. Ongeza vitendo ukipenda.
- Hapa ni mfano wa wimbo wa 'kunawa mikono' katika Kiingereza kwenye tuni ya 'happy birthday' (Heri ya siku ya kuzaliwa). Je, unaweza kuuimba?

  Wash hands well each day
  To keep germs away
  Scrub with soap and water
  And be on your way



**Umri**: Shule ya msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha, mdundo, silabi, maneno yenye vina.

**Mambo utakayojizoeza:** Mawasiliano, ubunifu.

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Ikiwa wewe ni kiziwi au una matatizo ya kusikia, unaweza kutunga nyimbo kwa lugha ya alama au za vitendo.
- Unaweza ukacheza wimbo kwenye redio na ukautungia maneno tofauti na yale ya asilia.
- Unaweza kucheza vyungu au ndoo huku mtu mwingine akiimba.

# Mashairi ya kipuuzi

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi


## Mambo ya kufanya:

- Angalia shairi la Kingereza la 'kipuuzi' lifuatalo ambalo lilitungwa na mshairi **Spike Milligan**. Unaweza kulikariri kimya kimya au kwa sauti ukitaka. Zingatia sana maneno yoyote ya kijinga au maneno yasiotarajiwa.

**On The Ning Nang Nong**

On the Ning Nang Nong
Where the Cows go Bong!
and the monkeys all say BOO!
There's a Nong Nang Ning
Where the trees go Ping!
And the tea pots jibber jabber joo.
On the Nong Ning Nang
All the mice go Clang
And you just can't catch 'em when they do!
So its Ning Nang Nong
Cows go Bong!
Nong Nang Ning
Trees go Ping
Nong Ning Nang
The mice go Clang
What a noisy place to belong

- Ukimaliza kusoma, shairi hili orodhesha **maneno yote ya kipuuzi** ambayo Spike Milligan alitumia katika shairi hili
- Je, ni neno gani la kipuuzi ninalokupendeza na kwa nini?
- Je, mnayo mashairi ya kipuuzi yoyote nchini au kwenye lugha yako?
- Tunga maneno ya kipuuzi yatakayowachesha marafiki zako
- Sauti ya kicheko? Miti inavyoonekana ikiwa mikubwa sana? Jina jipya la pua? Unaweza kukiitaje kitu kilicho na ladha mbaya sana? Sauti inayofanywa na miguu yako unapotembea katika majani yaliyokauka? Jina la aina mpya ya mnyama?
- Buni maneno yako mwenyewe matano mapya kisha uandike maana yake.
- Andika sentensi, shairi la kipuuzi au hadithi fupi kwa kutumia maneno yako. Huhitaji kuyatumia yote. Chagua yale unayoyapendelea zaidi na yale yanoyosikika vizuri zaidi yakiwa pamoja.
- Unaweza kutumia 'On the Ning Nang Nong' kama msukumo.. Jaribu kuanza mistari yako na vifungu sawa kama vile:
    - Kwenye ...
    - Ambapo...
    - Na ...










**Umri**: Miaka minane na zaidi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Kukuza lugha, fasili, muundo wa sentensi, vina na mdundo.

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, mawasiliano, kuunda maana

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Kariri au umwombe mtu akuandikie shairi lako.
- Andika shairi la mistari miwili.

# Panda mbegu na uiangalie inapokua

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Mbegu, udongo, maji, kifaa cha kuweka alama

## Mambo ya kufanya:

- Chagua aina ya mmea ambao ungependa kuotesha. Mharage, dengu au mbegu nyingine? Unataka kuotesha kitu kinacholiwa? Chunguza uone ni mbegu gani ambazo zinakomaa kua vizuri wakati huu wa mwaka na ni mbegu zipi zinapatikana.

- Amua mahali pa kupanda mbegu yako. Kwenye chungu au aridhini? Ukiamua kuipanda mbegu aridhini chagua pahali pasipokuwa na hatari ya mmea kusumbuliwa na wanyama. Chunguza ni pahali gani panapofaa zaidi kupanda mbegu yako. Katika eneo liliojengwa? Pamoja na kivuli au moja kwa moja kwenye miale ya jua?

- Panda mbegu yako katika eneo lisilo na magugu. Panda mbegu mbili au tatu kwenye shimo moja iwapo moja isipomea au chipuka (kua) Imwagilie maji vizuri.

- Tengeneza kielelezo cha mmea wako. Andika jina la mmea kwenye kijiti ukisimamishe kando na mbegu yako.

- Imwagilie kila siku au mara nyingi iwezekanavyo ili udongo ulowe

## Shughuli za ziada:

- Angalia ukuaji wake kila siku. Andika kumbukumbu za ukuaji wake. Pima mche kila siku unapomea/chipuka. Je, unachukua siku ngapi kabla ya kuota majani? Maua?



**Umri**: Miakaa yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Kulima, ulimwengu wa sasili, kutunza mmea

**Mambo utakayojizoeza:** Kuangalia, utatuzi wa matatizo

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Ukiwa na matatizo ya kutembea unaweza kupanda mbegu kwenye chungu ndani ya nyumba. Je! Unaweza kuufikia mmea wako ili uumwagilie maji? Je! uko katika mahali penye mwanga?
- Unaweza kukata sehemu ya juu ya chupa ya plastiki kutengeneza chungu.

# Kusoma pamoja

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Kitabu cha hadithi au unaweza ukatumia mojawapo ya hadithi zilizopo kwenye ukurasa unaofuata.

## Mambo ya kufanya:

- Ndugu mkubwa au mtu mzima anaweza kumsomea mtoto hadithi au ndugu mdogo anaweza kumsomea ndugu yake mkubwa au mtu mzima. Wakati mwingine, ni bora kufanya hivi kwa zamu na ili yote yafanywe yaani; mtoto aweze kumsomea mtu mzima na mtu mzima amsomee mtoto pia.
- Chagua hadithi (kutoka kwenye kitabu) ambayo nyote wawili mnapenda au tunga hadithi mpya. Inaweza kuwa hadithi halisi au ya kubuni.
- Kumbuka kubadilisha sauti yako wakati unasimulia. Unawezaje kuigiza sauti ya simba, mzee au ya sungura aliyeogopa?
- Kata hadithi wakati mwingine na uulize, 'unafikiri nini kitokea baadaye?' Jaribu kutabiri pamoja sehemu ya hadithi inayofuata.
- Katika ukurasa unaofuta kuna hadithi fupi mbili ambazo mnaweza kusoma pamoja.
- Mnaweza pia kusoma hadithi ya Fisi na Sungura kutoka kwenye shughuli, 'chora mnyama wa ajabu'. Soma sehemu kuu ya hadithi, sitisha kabla ya kusoma sehemu ya mwisho mjaribu kukisia namna itakavyoisha.
- Soma mwisho wa hadithi. Je, makisio yako yalikuwa sahihi? Unaweza pia kuipa hadithi hii kichwa?

### Shughuli za ziada:

- Mnaweza kuigiza pamoja mojawapo ya hadithi mnayoipenda. Amua utakuwa mhusika utakayekuwa kisha ufanye majaribio ya uigizaji/mchezo wako. Igiza hadithi yako kwa watu katika familia yako.

**Hadithi ya 1: Tembo, Ndovu:**

'Usiende mtoni' mama Ndovu alimtahadharisha mtoto wake Tembo kila mara. 'Kuna mamba mkubwa huko atakula' Tembo alikuwa na hamu ya kutaka kujua Mamba alikuwa nani? Hakuna mtu yeyote ambaye angemwambia. Kwa hivyo, alikwenda mtoni. Alisimama kwenye ukingo wa mto. Kisha akasogea karibu sana. Likini alichoweza kukiona ni uso wake kwenye maji mtoni. Alisogea karibu kidogo na ghafla …mamba alitokea akiwa na paya pana…Haraka haraka.

Alimshika Tembo kwa pua. 'Nisaidieni' Tembo alipiga kelele. Mama yake alikimbia kuelekea alikokuwa Tembo akashikilia mkia wake. Kaka zake walikuja huku wakikimbia wakashikiria masikio yake wakavuta lakini mamba hakuweza kumwachilia Tembo. 'Tusaidieni' waliita na kwa muda mchache kila mtu msituni akawa anavuta Tembo.

**Mwisho wake:**

Waliuvuta mkia wake ukawa mrefu kama Kamba, walivuta masikio yake yakawa makubwa, na pua lake likawa refu sana. Walivuta wakavuta na mwishowe mamba akamwachilia Tembo. Kila mtu alianguka chini juu ya mwenzake . Tembo alikuwa salama. Lakini nini kilitokea kwa mkia wake mdogo uliojipindapinda na masikio yake membamba, na …PUA lake je?

Hii ndiyo sababu kufikia siku hii, Ndovu wana pua ndefu zijulikanazo kama kama…na masikio makubwa yanayofanana kama kabichi.

**Hadithi ya 2: Matone Matatu ya Mvua (iliandikwa na Terry Jones):**

Tone la mvua lilikuwa likianguka kutoka kwenye mawingu likaambia tone lililokuwa karibu nalo "Mimi ni mkubwa na bora zaidi kushinda matone yote angani!"

'Kwa kweli wewe ni tone zuri sana la mvua', tone la mvua la pili lilisema, 'lakini hunishindi mimi urembo wa kisura. Kwa maoni yangu, sura ndiyo ya muhimu sana, na kwa hivyo mimi ndiye tone bora zaidi la mvua katika anga zima'.

Tone la kwanza likajibu: 'Hebu tutatulie suala hili mara moja' Hivyo basi, waliomba tone la mvua la tatu kuchagua na kuamua nani yuko bora zaidi kwa hao wawili. Lakini tone la tatu la mvua lilisema: 'ni upuuzi gani mnaouzungumzia nyie wawili! Unaweza kuwa tone kubwa la mvua, na kwa hakika umeumbika vizuri lakini kama kila mtu ajuavyo ya kwamba usafi ndio wa maana zaidi kwa kweli na mimi ninawashinda nyote kwa safi. Kwa hivyo mimi ndiye tone la mvua lililo bora zaidi angani!

**Mwisho wake:**

Kabla ya tone lolote kuweza kujibu , matone yote yalianguka chini yakawa sehemu ya dimbwi la matope.

**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mkubwa

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha, muundo wa hadithi, utabiri na drama

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, kazi ya pamoja, ushirikiano, kusikiliza

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Unaweza kusimulia hadithi kwa kutumia lugha ya ishara. Kumbuka kutumia sana ishara uso. .
- Igiza hadithi kwa kutumia karagosi za soksi.

# Windo la skavenja

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Karatasi na penseli

**Mambo ya kufanya:**

- Windo la skavenja ni mchezo ambao mchezaji anapaswa kwenda kutafuta vitu vilivyoandikwa kwenye orodha. Unaweza 'kuviwinda' ndani au nje. Ukifanya windo na watu wengine, mtu anayetangulia kupata kila kitu kwenye orodha ndiye mshindi.
- Angalia orodha. Unaweza kukusanya vitu vyote vilivyoko kwenye orodha kwa haraka kiasi gani ukiwa peke yako au na wengine?

    - Kitu chenye rangi ya blu
    - Kitu laini
    - Vitu viwili vinavyotengenezwa kutokana na mbao
    - Chakula/kinywaji kitamu
    - Vitu vitano vinavyoanza na herufi sawa
    - Kitu kinachongaa
    - Kitu kinachotumiwa kusafisha
    - Kitu unachopenda

- Ikiwa ulicheza mchezo wa kuwinda skaveja na mtu mwingine. Linganisha vitu ambavyo nyote wawili mmekusanya.
- Sasa unda orodha yako mwenyewe. Utumiaji wa vivumishi (laini, tamu, ang'aa) na rangi ni mwanzo mzuri. Angalia mifano mingine hapo juu uone ikiwa unaweza kutengeneza orodha yako mwenyewe ya vitu 10 vya kutafuta.

- Andika orodha yako na umwombe mtu mwingine kutafuta vitu hivyo.




**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha (vivumishi na majina), kuhesabu

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, utatuzi wa matatizo, ushirikiano

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**


- Chagua vitu kutoka chumba kimoja nyumbani kwako.
- Onyesha vitu na uombe mtu fulani akusaidie kukupatia vitu hivyo.
- Sema au umsomee mtu mwingine kwa sauti vitu unavyotaka yeye akuandikie katika orodha.
- Ukiwa na matatizo ya kuona, unaweza kumwomba mtu fulani kukusanyia vitu kutafuta vitu viwili viwili na kuvificha kwenye chumba. Matakia/Mito miwili? Vitabu viwili? Viatu viwili?

# Alama ya siri

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi.

## Mambo ya kufanya:

- Kuna njia nyingi za kuunda alama yako ya siri iliyoandikwa.
- Unaweza kubadilisha kila herefu katika alfabeti yako na nambari lakini anza na nambari ya juu na uziorodheshe kwa kurudi nyumba, Kwa mfano, Lugha ya Kiingereza ina herufi 26 za kialfabeti, kwa hivyo, **a=26, b=25, c=24, d=23 n.k.** Unaweza kutambua alama hii inachosema? **8 22 24 9 22 7 24 12 23 22**
- Unaweza ukabadilisha kila herufi na herufi nyingine ya kialfabeti lakini hakikisha ya kwamba zinabaki katika mpango wa kialfabeti, kwa mfano **a=h, b=i, c=j, d=k, e=l, f=m n.k.**




- Unaweza kuiundia alama mpya kila herufi ya kialfabeti kama ilivyo katika mfano. Ukiamua kuunda alama zako, jiulize maswali yafuatayo:

    - Je, alama zangu za siri ziandikwe kwa mpangilio wa kushoto kwenda kulia au wa kutoka juu kwenda chini?

    - Je, niwe na idadi sawa ya ishara kama idadi ya herufi katika alfabeti? Au ishara chache zinazowakilisha herufi moja? (Jambo hili linaifanya alama yako ya siri kuwa ngumu sana kwa watu wengine kuivunja.

- Unaweza kutunga maneno katika Kingereza kulingana na ishara ulizopewa kwenye ukurasa uliotangulia? (kumbuka, huna alama ya siri yote!!)



- Tayarisha kalamu/penseli yako. Andika alama yako ya siri kiukamilifu. Halafu uandike jumbe zako za siri uone kama watu wengine wanaweza kuzifumbua.

**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ubunifu, mawasiliano, utatuzi wa matatizo

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, mawasiliano, utatuzi wa matatizo

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Ukiwa na matatizo ya kuona, unaweza kuunda alama yako ya siri ya maneno tu. Chagua sauti kama 'ka', 'ub' au 'sha'. Tanguliza sauti hiyo kabla ya kila neno au hata kabla ya kila silabi. Kwa mfano ukisema "I am happy (Nimefurahi)" kwa Kiingereza inaweza kusikika kama "kai kam kahap kapy'.

# Maumbo na mikondo katika ulimwengu wa asili

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Vijiti na mawe

## Mambo ya kufanya:

- Toka nje. Je, unaona maumbo na mikondo mingapi katika ulimwengu wa asili? Pia, anagalia vitu vinavyotoka kwenye ulimwengu wa asilia mlivyo navyo nyumbani kwako, kama vile matunda na mboga.




- Unaweza kutaja maumbo na mikondo mingapi tofauti? Je, unaweza kupata kitu ambacho:
  - Ni cha ulinganifu?
  - Kina mpangilio wa mzunguko?
  - Ni duara au tufe?
  - Inaonekana kurudia ruwaza sawa mara nyingi?
  - Ni ya sura ya nyota au moyo?

- Je, umetambua ya kwamba baadhi ya majani yanaonekana kama miti ya kisanamu? Unaweza kupata jani kama hili? Unaweza kuhesabu idadi ya sehemu ndogo kwenye shina kuu la jani?

- Kusanya vijiti na mawe. Unaweza kutengeneza maumbo gani mengine na vitu hivyo? Je, unaweza kutengeneza:

  - Pembe tatu au mraba,
  - Pembetano (umbo lenye pembe tano),
  - Pembe sita (umbo lenye pembe sita),
  - Pembe nane (umbo lenye pembe nane)



- Unaweza kuunda au kutengeneza maumbo yoyote ya pande tatu kwa kutumia vijiti vyako na mawe? Piramidi au kimchemraba kwa mfano?

**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Majina ya maumbo, maneno ya kuelezea mikondo, kuhesabu

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, utatuzi wa matatizo, kushirikiana, ucchunguzi

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Je, unaweza kutembea kwenda kwa jirani yako, ikiwa huna sehemu ya nje karibu na nyumbani kwako?
- Je, mtu mwingine anaweza akakupa trei ya vitu na vifaa vya kuchunguza ikiwa una matatizo ya kutembea?

# Duala la hadithi

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi

**Mambo ya kufanya:**

Unaweza kufanya shughuli hii na watu watatu au zaidi. Kaeni pamoja katika duala.

- Mtu mmoja anaanza hadithi, kwa mfano, "**Kulikuwepo msichana mdogo ambaye alikosa usingizi.Alijigeuza geuza huku na pale lakini hakupata usingiza**".

- Malizia hapa. Omba mtu anayefuata katika duala aendeleze hadithi katika sentensi moja au mbili, kwa mfano: "Aliendekea kuutazama mwezi mkubwa wenye umbo la duara. Ghafla kitu fulani kilionekana kutembea kutoka mwezini kwelekea alikokuwa. Kitu hicho kilikuwa ngazi ya fedha iliyoshuka chini, chini, chini kuelekea kwa dirisha lake"

- 'Ruka zamu' ya kwendeleza hadithi kwa mtu mwingine kwenye duara. Unaweza kuendeleza hadithi kwa muda gani? Ikiwa kuna watu wawili tu kwenye duara, simulia hadithi kwa zamu.

- Omba mtu mmoja ahitimishe hadithi baada ya kila mmoja wenu kusimulia kwa angalau zamu mbili.

- Sheria za mchezo wa kusimulia hadithi kwenye duara ni:
  - Tumia mawazo yako, kila kitu kinawezekana!
  - Pendeleza hadithi mbele (unaweza kusema, alipanda ngazi' kisha usitishe, unapaswa kusema mengi zaidi 'alipanda ngazi hadi alipofika kileleni akaona…').
  - Usisimulie hadithi nzima, mwache mtu anayefuata aiendeleze hadithi.

- Unaweza kuchagua aina yoyote ya hadithi. Inaweza kuhusu jambo la kweli/halisi (sherehe au safari) au mnyama au hadithi ya kubuni kutokana na mawazo yako.



**Umri**: Shule ya msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha, muundo wa hadithi na kanuni za hadith: mambo unayoweza kufanya au kotofanya katika hadithi unapoanza kuisimulia.

**Mambo utakayojizoeza:** Kufikiri haraka, ubunifu, mawasiliano na ushirikiano.

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Weka vitu 10 kutoka nyumbani kwako kwenye begi- kila kitu unachoweza kupata, (kwa mfano kikombe, jiwe, kitambaa). Ondoa vitu begini kwa zamu, kila wakati unapochukuwa kitu kipya kitumie kukusaidia kuongezea sentensi moja au mbili kwenye hadithi. Kwa mfano, 'juu ya ngazi msichana huyo aliona kikombe, kikombe cha dhahabu na kilikukuwa kinafulika na kioevu cha ajabu cha dhahabu…'.
- Andika hadithi nzuri mliyotunga pamoja. Ongezea vivumishi na lugha ya maelezo kuifanya iwe hadithi ya kupendeza sama.

# Shukuru shujaa wa Jamii

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Karatasi na penseli

## Mambo ya kufanya:



- Shujaa wa jamii anaweza kuwa mtu yeyote wa kawaida ambaye amesaidia watu wengi au yule aliyekuwa na ujasiri wa kusonga mbele licha ya kukumbana na changamoto nyingi. Mtu yeyoye anaweza kuwa shujaa. Je, unajua mtu yeyote kama huyu?
- Fikiria nguli/shujaa wa jamii yako. Je, yeye ni mtu gani? Je, alifanya nini? Kwa nini unampenda?
- Je, unataka kumshukuru vipi shujaa wako? Kwa kutumia mchoro, bango au wimbo wa kushereherekea mafanikio yake? Barua ya asante au zawadi nyingine? Au labda unataka kusema tu 'Asante au shukrani'.
- Andaa zawadi yako/andika barua yako kisha tafuta njia ya usalama ya kuipeleka barua hiyo kwa shujaa wako.

**Umri:** Shule ya Msingi

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Kuelewa Muundo wa lugha

**Mambo utakayojizoeza:** Mawasiliano, ubunifu, kuwa na huruma na uwezo wa kuhisi maono ya watu wengine.

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Mwombe mtu mwingine akusaidie kukuandikia barua yako ukimwambia yale unayotaka yawe ndani ya barua yako. Chora picha utakayotuma na barua hiyo au weka zawadi.

# Kuwinda hazina

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Penseli au kalamu na karatasi

## Mambo ya kufanya:

Kuwinda Hazina ni mchezo ambao wachezaji hutafuta vitu vilivyofichwa kwa kufuata vidokezo/kudokezea. Kila kidokezo unachomalizia hukuongoza kwa kidokezo kingine hadi unapopata hazina. 'Hazina' ya mwisho inaweza kuwa kitu chochote unachotaka- Kitu kidogo cha kupendeza au kitu cha kula (hakikisha ya kwamba mnyama hakutangalia kukipata!)

- Fikiria **jinsi ungependa kufanya uwindaji hazina kwa** – ndugu yako mdogo au mkubwa? Mtu mzima? Utahitaji kuandika vidokezo vinavyofaa umri wao na zile wanazoweza kufahamu (angalia baadhi ya mifano hapa chini).
- Fikiria juu y**a ni wapi unataka kufanya uwindaji hazina** – ndani au nje au yote mawili? Je, uwindaji hazina utaanzia na kuishia wapi?
- Chagua **maeneo ambapo vidokezo vya uwindaji hazina** (mahali vidokezo vikakowekwa) Mti mkubwa? Kabati kwenye nyumba, au kidokezo anaweza kuwa mtu mmoja katika familia ambaye hatashiriki kwenye mchezo. Maeneo kama 8 yanatosha. Andika maeneo na uyawekee nambari kwa mpango. .
- Andika vidokezo ya kila eneo kwenye karatasi nyingine. Hakikisha kwamba vidokezo hivi vinaweza kueleweka kwa 'wachezaji' lakini usivirahihishe sana! Kwa mfano:
  - Kidokezo: Nina mchungwa mtamu, tunda lenye mnato (Mahali maalum: mwembe)
  - Kidokezo: Thapa ni mahali unapootea usiku (Mahali maalum: kitanda)

- Unaweza pia kutumia anagram (pale unapounda neno kwa kubadilisha herufi za neno jingine) kwa mfano:
  - Kidokezo: ODON AY JAMI (Eneo: Ndoo ya maji)
  - Au unaweza kutumia alama ya siri (nywira)

- **Viwekee nambari vidokezo** uvikunje ili kuonekane nambari peke yake. Utawapa wachezaji kidokezo cha kwanza ambacho kitawaongoza kwa kidokezo kingine kuendelea.

- **Hifadhi kidokezo cha kwanza ufiche vidokezo vingine** katika maeneo katika mpangilio sahihi- tumia orodha ulioandika awali kukusaidia kukumbuka mahali pa kuvificha. Ficha nambari ya pili kwenye kidokezo cha nambari ya kwanza . Kwenye kidokezo cha nambari ya 2 ndiko utakakoficha nambari ya 3 na kadhalika. Utaficha 'hazina' kwenye kidokezo cha mwisho.

- Ikiwa kuna wachezaji zaidi ya mmoja, **mkubaliane kuhusu sheria za mchezo pamoja** Baadhi ya sheria zinaweza kuwa kwa mfano:
  - Tunahitaji kungojeana kabla ya kwenda kwa dokezo linalofuata.
  - Tunahitaji kuchukua zamu ili kufumbua kidokezo
  - Tunahitaji kugawana hazina tunapoipata.

- **Kabidhi kidokezo cha kwanza** Tembea na mchezaji/wachezaji ikiwa wamekwama na wanahitaji usaidizi wa ziada kuelewa vidokezo.

**Umri**: Miaka kumi kuendelea

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Wastani

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha, kuandika na tahajia

**Mambo utakayojizoeza:** Kupanga vitu, utaratibu, ubunifu, umakinifu, mawasiliano, ushirikiano, utatuzi wa matatizo

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Omba mtu mwingine akusaidie kuandika vidokezo.
- Andika vidokezo 3 au 4 tu
- Usicheze mchezo wa kuwinda hazina kama 'njia'lakini kila kidokezo kinaweza tu kukuongoza kwa 'hazina ndogo'- hii inarahihisha uanzishaji wake.
- Rahihisha vidokezo kwa kuchora picha.

# Maswali ishirini

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Hakuna

## Mambo ya kufanya:

Shughuli hii hufanyika vizuri zaidi baina ya wachezaji wawili hadi watano ili kila mtu apate nafasi ya kuuliza swali.

- Unaweza kuchagua mtu yeyote katika kundi lako kutangulia kucheza, kwa mfano mdogo kuliko wengine, au mtu aliyesheherekea siku yake ya kuzaliwa hivi karibuni.
- **Pchagua mtu, mahali au kitu.** Fikiria juu ya mtu au kitu unachojua sana kujibu maswali ya msingi yanayokihusu au yanayomhusu mtu huyo. Ikichagua mtu, anaweza kuwa bado anaishi au aliaga dunia, au pia wa kubuni (kutoka kwenye hadithi). Hakikisha kwamba unachagua mtu,mahali au kitu ambacho watu wengi kutoka kwenye kundi lako wanajua. .
- Usimwambie mtu chaguo lako bado. Mwache abahatishe ulichochagua.
- Maswali mengine, uliza maswali yanayohitaji majibu ya ndiyo au hapana. Anza na swali la jumla lililowazi ambalo linaweza kujibiwa kwa 'ndiyo' au 'hapana'. Kwa mfano:
    - "Je, ni mtu?"
    - "Ni mahali ?"
    - "Ni kitu?"
    - "Ni ya kweli au ni ya kubuni?"



- Chukua zamu ya kuuliza maswali ya ndiyo au hapana. Hakikisha kuwa kila mchezaji anapata fursa ya kuuliza angalau swali 1. Ikiwa

mchezaji anauliza swali ambalo haliwezi kujibiwa kwa "ndiyo" au "hapana," mwombe afafanue tena ili liweze kuwa. Kwa mfano, mchezaji hakuweza kuuliza, "Wana umri gani?" lakini wangeweza kuuliza, "Je! wana umri zaidi ya 50?"

- **Uliza Maswali mahsusi zaidi unapoendelea.** Fikiria juu ya maswali ambayo yameulizwa tayari kabla ya kuuliza maswali mapya. Kwa mfano, ikiwa mtu tayari ameuliza juu ya ukubwa, endelea uulize kuhusu rangi au nyenzo kitu hicho kimetengenezwa.

- **Cheza hadi ufikie maswali 20 au mtu atoe jibu sahihi.** Hesabu maswali pamoja. Kundi likifika maswali 20 na hawajatabiri/bahatisha mtu, mahali au kitu, wape jibu. Mchezo unaisha, mtu akibahatisha kabla maswali 20 yameulizwa.

- **Mfanye mtu aliyetoa kiabashiri sahihi anayefuata kucheza** Ikiwa hakuna yeyote aliyebahatisha mtu, mahali au kitu sahihi, mtu yeyote anayetaka kucheza anaweza kuchukuwa zamu hiyo. Wacha kila mtu apate nafasi ya kufikiria kitu. Kumpa kila mtu zamu huufanya mchezo wa kujumuisha watu wote na kumpelekea kila mtu kufurahia/kuburudika!

**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha, aina/makundi

**Mambo utakayojizoeza:** Mawasiliano, umakinifu, utatuzi wa matatizo

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**


- Dhibiti maswali kwa kategoria maalumu k.m. 'wanyama', 'chakula' au watu maarufu'. Wambie wachezaji ni hiyo ni kategoria gani.
- Chezeni katika timu ya watu wawili ili muweze kusaidiana katika jozi yenu.
- Panua mchezo zaidi ya maswali ishirini ili uwe na nafasi zaidi ya kupata jibu sahihi.
- Weka vitu kama ishirini kutoka karibu na nyumbani kwako kwenye meza au kwenye trei. Chagua kitu kimoja kwa siri. Wengine wanapaswa kubahatisha ni kipi ulichochagua.

# Barua kwa mwalimu wako

**Zana utakazohitaji kuwa nazo:** Karatasi na Penseli

## Mambo ya kufanya:

- Andaa penseli na karatasi.
- Fikiria juu jambo unalopenda kumwambia mwalimu wako. Je, unataka kumwambia kuhusu kazi unazofanya nyumbani? Unaweza kuzungumzia:
  - Jambo ambalo umefurahia
  - Jambo la kuchekesha lililotokea
  - Jambo gumu ambalo umefanya
  - Kitu unachotarajia kupata/kufanya
- Andika barua yenye anuani na tarehe uitie sahihi.
- Ikiwezekana, unaweza kuipeleka barua kwa mwalimu wako salama salimini? Omba mtu mzima au ndugu yako mkubwa akusaidie kuipeleka barua hiyo kwa mwalimu.


Dear mrs roper,
I tryed Joe wicks and i loved it. It was funny when me and my mum got tangled up in the swing ball. I also tryed maths game, and all the different games on it. Some of them are difficult and some of them are really fun!. I'm looking forward to making something out of wood. yours

sincerely

Theo:

**Shughuli za ziada:**

- Je, unaweza kuiandikia jibu la kufikiria la barua kutoka kwa mwalimu wako? Tumia maneno ambayo mwalimu wako angetumia.

- Unaweza kumwandikia mwalimu wako barua ya kuchekesha ukielezea sababu iliyokupelekea kukosa kufanya zoezi lako la kufanyia nyumbani? Fikiria udhuru wa ajabu, kwa mfano:

    - "mbuzi alikula zoezi langu".

    - "upepo ulikuwa mkali sana ukaipeperusha kazi yangu".

- Tumia kiolezo hiki kukusaidia kuandika barua yako.

Tafadhari nisamehe kwa kutofanya zoezi langu la kufanyiwa nyumbani.

Samahani sana lakini... (je, kulitokea nini?) ....

Nita...(Je,utafanya nini?)..........

Kila la Heri,

Sahihi:



**Umri**: Miaka yote

**Usaidizi wa Mtu mzima/Ndugu:** Mdogo

**Mambo utakayojifunza:** Ukuzaji wa lugha, uandishi wa barua, muundo wa sentensi, tahajia

**Mambo utakayojizoeza:** Ubunifu, huruma au uwezo wa kuhisi maono ya watu wengine

**Njia tofauti za kufanya shughuli:**

- Msomee mtu mwingine barua yako kwa sauti (Mwombe akusaidie kuandika).
- Andika barua fupi.
- Mchoree mwalimu wako mchoro wa vitu unavyofanya nyumbani.